

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: **"TUME"**
DAR ES SALAAM
Namba ya Simu: 2460117
Fax: 255 - 022 - 246011
e-mail: Secretary@psc.go.tz
Website: www.psc.go.tz



TUME YA UTUMISHI WA UMMA,
UBUNGO PLAZA,
BARABARA YA MOROGORO,
S.L.P. 9143,
DAR ES SALAAM.

TAARIFA KWA UMMA.

Tume ya Utumishi wa Umma inapenda kuwataarifu Watumishi wa Umma na Wananchi kwa ujumla kuwa, katika kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2018 imetenga siku tatu (3) mahsusi kwa ajili ya kupokea na kuyatolea ufafanuzi **Malalamiko na Kero** kutoka kwa wadau wake kuhusu masuala ya usimamizi wa Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma.

Zoezi hili la kukutana na wadau wa Tume linafanyika tarehe 20 hadi 22 Juni, 2018 kuanzia saa 3:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni katika Ofisi ya Tume iliyopo Ghorofa ya Saba, kwenye Jengo la Ubungo Plaza, Barabara ya Morogoro jijini Dar es Salaam.

Aidha, kwa wadau watakaoshindwa kufika katika Ofisi za Tume, bado wanayo nafasi ya kuwasilisha Kero au Malalamiko kwa njia ya barua kwa **Katibu, Ofisi ya Rais - Tume ya Utumishi wa Umma, S.L.P. 9143 Dar es Salaam.** Au kwa barua pepe: secretary@psc.go.tz.

"WADAU WOTE MNAKARIBISHWA"

Imetolewa na:-


Richard M. Odongo

KAIMU KATIBU

TUME YA UTUMISHI WA UMMA